

UWATA SHULE YA AWALI NA MSINGI MCHIEPUO WA KIINGEREZA

Tel: +255-25-2510051

Mobile: +255-763-674878

+255-754-432411

Fax: +255-25-2510341



S.L.P. 3574,
MBEYA

Email: uwataprimarys@yahoo.com

FOMU YA USAILI (INTERVIEW) YA KUJIUNGA NA SHULE MSINGI UWATA (Gharama ya fomu ni 25,000/=)

NAMBA YA FOMU: _____

A: MAELEKEZO YA AWALI

1. Fomu hii ijazwe kwa herufi kubwa.
2. Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi anayetaka kujiunga na shule ya msingi.

Picha ya Mzazi

Picha ya
Mwanafunzi

B : HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi
2. Umri wa mwanafunzi Jinsia yake MV/MS:
3. Mahali anapoishi WILAYA: MKOA:
4. Darasa analo omba
5. Lugha atakayojibia Mtihani: (Kiingereza/Kiswahili)

C: HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi
2. Kazi anayofanya
3. Mahali anapoishi
4. Anuani ya Mzazi/Mlezi
5. Namba ya simu: Mkononi Kazini :.....
Nyumbani :

D: MAELEKEZO MUHIMU

- Usaili utafanyika siku ya jumamosi tarehe 03/12/2016 kuanzia saa 2:00 asubuhi na mwanafunzi atakayechelewa zaidi ya nusu saa hataruhusiwa kuingia.
- Kituo cha usaili ni kimoja tu, yaani uwata shule ya msingi. Na matokeo yatatolewa siku tatu baada ya mtihani yaani Jumatatu tarehe 5/12/2016.
- Baada ya kufaulu na kufahamishwa kuwa amepata nafasi Mzazi/Mlezi utachukua fomu ya maelekezo (Joining instruction) kwa Tsh.15,000/=), fomu zitatolewa kuanzia Jumatatu tarehe 05/12/2016 mpaka ijumaa tarehe 09/12/2016, endapo mzazi/mlezi utashindwa kuchukua fomu kwa muda huo basi nafasi hiyo atapewa mwingine..
- Mwanafunzi anayeomba nafasi ya darasa la I,II & III atatakiwa kufanya usaili katika somo la HESABU, KIINGEREZA, KISWAHILI, SAYANSI, KUSOMA NA KUANDIKA.
- Mwanafunzi anayeomba nafasi ya darasa la IV,V & VI atatakiwa kufanya usaili katika somo la HISABATI, KIINGEREZA, KISWAHILI, SAYANSI na MAARIFA YA JAMII.
- Mitihani imeandaliwa kwa lugha mbili; Kiingereza na Kiswahili, mwanafunzi atachagua lugha anayoweza.
- Siku ya ushahidi Mzazi/Mlezi unapaswa kuleta kivuli cha cheti cha kuzaliwa cha mtoto na kiambatanishwe na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu na kubandikwa picha ya mzazi/mlezi na mwanafunzi.
- Mwanafunzi anayeomba nafasi ya shule ya msingi darasa la I, II, III, IV na V endapo atachaguliwa kujiunga na shule yetu atapewa nafasi ya kutwa kwa usafiri binafsi, kutwa kwa usafiri wa shule au bweni kulingana na matakwa ya mzazi. Mwanafunzi anayeomba darasa la VI atatakiwa kukaa bweni na si vinginevyo.

E: SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

1. Mtoto haruhusiwi kusuka nywele
2. Mtoto atapokelewa hapa shuleni iwapo hana magonjwa ya kuambukiza.
3. Huruhusiwi kumwachia mtoto kiasi chochote cha fedha mkononi mwake au kumletea chakula mwanafunzi wa bweni
4. Mwanafunzi anapaswa kuongea kiingereza awapo shuleni isipokuwa kwenye somo la Kiswahili.

5. Kila mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu watu wote.
6. Mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni kwa muda unaotakiwa.
7. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuvuta sigara,kunywa pombe na kutumia madawa ya kulevya, kutukana matusi, kupigana na kujihusisha katika vitendo vya mapenzi na adhabu yakufukuzwa shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na vitendo vya kishirikina kwa maneno au matendo. Pia kuvaa hirizi na kutumia madawa yasiyo thibitishwa na daktari.
9. Kila mwanafunzi ni lazima kuhudhuria vipindi vya ibada, neno la mungu na maombi bila kujali tofauti ya dini ya mwanafunzi husika kwani shule hii ni ya kikristo.
- 10.Mwanafunzi atokapo nje ya shule ni sharti avae sare za shule.
- 11.Ni marufuku mwanafunzi kuharibu mali za shule, mara ikibainika kufanya hivyo kwa makusudi mzazi/mlezi atatakiwa kulipa fidia kwa mali hizo.

MOTTO WA SHULE '***ELIMU NI UKOMBOZI***'

E. ABEL

MKUU WA SHULE